

# AFICAT kukuza matumizi ya teknolojia za kisasa katika zana za kilimo nchini



Uasilishaji wa kampuni ya Honda kwa Mkoa wa Kilimanjaro.

**K**atika Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Maendeleo ya Afrika wa Tokyo (TICAD7) uliofanyika Yokohama, Japan, mwaka 2019, Kituo cha Uvumbuzi cha Afrika kwa ajili ya Teknolojia ya Kilimo (Africa Field Innovation Center for Agricultural Technology -- AFICAT) kilipendekezwa kuanzishwa katika nchi za Afrika kwa ajili ya kukuza teknolojia ya hali ya juu ya zana za kilimo, kwa ubia wa sekta ya umma na binafsi kati ya Japan na Afrika.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, ambaye aliwakilisha Tanzania katika mkutano huo wa TICAD7, alitoa shukrani zake kwa Japan kwa kutoa ushirikiano katika nyanja mbalimbali kama vile kilimo, elimu, maji, miundombinu na michezo. Pia alitumia fursa hiyo

kueleza matarajio yake ya dhali kutoka katika uwekezaji wa Japan nchini Tanzania.

Kutokana na hali hiyo, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA) limekuwa katika majadiliano na Wizara ya Kilimo (MoA) na mashirika mengine yanayohusika nchini Tanzania, na kutambua Kituo cha Mafunzo ya Kilimo cha Kilimanjaro (KATC) cha wizara na maeneo ya Skimu ya Umwagilaji ya Moshi Chini, ambayo yameanzishwa na kuwezesha na ushirikiano huo wa Japan tangu miaka ya sabini, kama msingi wa AFICAT nchini Tanzania. Wataalamu wa Kijapani wametumwa nchini kuanza majaribio ya miradi hiyo mwezi Machi 2022.

Tangu AFICAT ihimise matumizi ya zana za kisasa za kilimo, ambayo ni moja ya maeneo ya kipaumbele katika Mkakati wa Kitaifa


wa Maendeleo ya Mpunga (NRDS) wa Wizara ya Kilimo, inatarajiwa kuwa mpango huo utachangia katika utekelezaji unaoendelea wa awamu ya pili ya NRDS ambayo inalenga kuongeza uzalishaji wa mpunga nchini kutoka tani milioni 2.2 za sasa hadi tani milioni 4.4 ifikapo mwaka 2030.

AFICAT itaisaidia Tanzania kujitegemea kwa mpunga, na kuwa tegemeo la nchi nyingine za Afrika.

Timu ya wataalamu ya Japan ya AFICAT inakaribisha kampuni za nchi hiyo, wafanyabiashara wa Tanzania, na taasisi zinazohusika na sekta hiyo, kuleta, kuthibitisha, na kutambulisha teknolojia na bidhaa za Kijapani. Tayari kampuni ya Honda Motor Co., Ltd ambayo ndiyo kubwa zaidi ya kutengeneza pikipiki duniani, kwa mfano, sasa inatambulisha bidhaa zake za umeme kama vile tiller, pump, sprayer, na brush cutter nchini kwa kushirikiana na AFICAT.

Timu hiyo inapanga kuwasilisha maendeleo ya shughuli za AFICAT nchini na nchi nyingine za Afrika kwenye mkutano ujao wa TICAD 8 utakaofanyika Tunisia Agosti 27 na 28, 2022. Baada ya hapo, timu ya wataalamu itaendelea na shughuli zao za majaribio nchini Tanzania na kupendekeza mpango wa shughuli wa muda wa kati na mrefu wa AFICAT kwa ajili ya utekelezaji endelevu wa shughuli zake kulingana na mafunzo waliyoyapata kutoka katika majaribio ya awali.

Kama mojawapo ya kanuni za kuanzisha AFICAT, kazi za msingi, kama inavyoonyeshwa kwenye takwimu hapa chini, zinapaswa kuelekezwa katika miundombinu na taasisi zilizopo badala ya kujenga miundombinu mipya. Inatarajiwa kuwa, KATC itakuwa kitovu cha ubora wa zana za kilimo nchini, hususan cha mpunga.



Kama unahitaji maelezo zaidi kuhusu AFICAT, tafadhali wasiliana nao kupitia:  
**Ofisi za JICA Tanzania:**  
 Andrew-Ridda@jica.go.jp  
**Makao Makuu ya JICA:**  
 aficat@jica.go.jp  
**Timu ya wataalam wa AFICAT ya JICA:**  
 aficat.team@kmcinc.co.jp



## Faida kubwa zitokanazo na AFICAT Tanzania

- Uwezesaji wa zana za kilimo na uanzishaji wa teknolojia za hali ya juu kuanzia katika utayarishaji wa ardhi hadi usimamizi baada ya kuvuna utakaofanywa na kampuni na teknolojia za Kijapani.
- Kwa kutekeleza uhakiki, maonyesho na majaribio ya teknolojia ya kijapani, maafisa wa serikali na wataalamu watapata mafunzo ya jinsi ya kutumia mashine katika kilimo
- Uzalishaji na ubora wa mpunga na mazao mengine hatimaye unaborehwa, na mapato ya wazalishaji na wasindikaji wa mazao haya yanaimarishwa kulingana na sera na programu zinazohusu kilimo za Tanzania.